**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule, 0764876455**

**Makamu Mkuu wa Shule, 0745905369**

**Matron/Patron,0762575544,0766305472**

**Shule ya Sekondari MAZWI**

**S.L.P. 632**

**Tarehe 12/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**

**..................................................**

**S.L.P ..........................................**

**..................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAZWI HALMASHAURI YA SUMBAWANGA MKOA RUKWA MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2023/2024** na atasoma tahasusi ya **HGK/HKL**

Shule ya Sekondari Mazwi ni **Kutwa** na ipo umbali wa Mita **5** Kusini mwa stendi kuu ya mabasi (**stendi ya sokomatola**) katika Mji wa Sumbawanga mjini.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **3/7/2023**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **26/6/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **01/7/2023**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili(2) rangi ya damu ya mzee zote kwa Wasichana na suruali mbili(2) za damu ya mzee zote kwa Wavulana.
ii. Shati mikono mirefu nyeupe mbili(2).
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni damu ya mzee,(ifanane na rangi ya sketi) ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Vazi la tai iendane na sketi na suruali na iwe moja.
v. Sare ya Michezo ni traki suti, rangi ya bluu bahari yenye ufito mweupe, kwa wasichana na wavulana na raba jozi moja Kwa wasichana na wavulana.
vi. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vii. Soksi jozi mbili rangi nyeupe.
viii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
ix. Sweta rangi ya bluu.
x. Tisheti (T-shirt).

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari kumi(10) ziwe kwaya 3 na zaidi;
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv. Ndoo 1 ndogo (lita Kumi) yenye mifuniko;
v. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mfagio 1 (mgumu).

**Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

**Michango yote ilipwe kupitia A/C namba 62102300019 (NMB), Jina la A/C ni ELIMU YA KUJITEGEMEA MAZWI SEKONDARI.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
viii. Kutunza mali za shule;
ix. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
x. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ..........................................

**Jina la Mkuu wa Shule** ...GODSON G. MWAIBINGILA...

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ...THE HEADMASTER MAZWI SECONDARY SCHOOL P O BOX 632 SUMBAWANGA...

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0764876455**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0745905369**
- **Mwandamizi Taaluma 0628141813**
- **Mwandamizi Malezi 0752196833**